



AZIMIO NA. 6/2014

**AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA UZUIAJI WA
VITENDO HARAMU DHIDI YA USALAMA WA MIUNDOMBINU YA
KUDUMU ILIYOJENGWA CHINI YA BAHARI KATIKA MWAMBAO
WA BARA YA MWAKA 1988 (*"THE PROTOCOL FOR THE
SUPPRESSION OF UNLAWFUL ACTS AGAINST THE SAFETY
OF FIXED PLATFORMS LOCATED ON THE CONTINENTAL
SHELF – SUA PROTOCOL 1988"*)**

KWA KUWA, Tanzania ni Mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization – IMO) na Umoja wa Kudhibiti Fedha Haramu kwa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (*Eastern and Southern Africa Anti Monetary Laundering Group – ESAAMLG*);

NA KWA KUWA, Mwezi Mei, 2005 Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo Viovu dhidi ya Usalama wa Usafiri Majini wa Mwaka 1988 (*Convention for the Suppression of Unlawful Acts against the Safety of Maritime Navigation, 1988*) ambao ulianza kutumika rasmi tarehe 9 Agosti, 2005;

NA KWA KUWA, Mwaka 1988 Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organisation – IMO) liliandaa Itifaki ya Uzuiaji wa Vitendo Haramu dhidi ya Usalama wa Miundombinu ya kudumu iliyojengwa chini ya Bahari

katika Mwambao wa Bara yaani *“Protocol for the Suppression of Unlawful Acts against the Safety of Fixed Platforms located on the Continental Shelf, 1988”*;

NA KWA KUWA, Tanzania pia imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo Viovu dhidi ya Usalama wa Usafiri Majini wa Mwaka 1988 ambao ni sharti la msingi la kuridhia Itifaki ya Uzuiaji wa Vitendo Haramu dhidi ya Usalama wa Miundombinu ya kudumu iliyojengwa chini ya Bahari katika Mwambao wa Bara ya Mwaka 1988;

NA KWA KUWA, Itifaki hii inaitaka kila nchi mwanachama wa Itifaki kuwa na mikakati ya kulinda usalama wa miundombinu na maisha ya Watu walioko kwenye miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na kuweka adhabu kulingana na aina ya uhalifu ulioainishwa katika Itifaki hii kulingana na mamlaka yake ya kisheria;

NA KWA KUWA, kujiunga na Itifaki hii, Tanzania itafaidika kutokana na kuimarika kwa usalama wa miundombinu ya kudumu iliyojengwa chini ya Bahari katika Mwambao wa Bara pamoja na maisha ya Watu wanoishi au kufanya kazi kwenye miundombinu hiyo, pamoja na kusaidia kudhibiti biashara ya fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya kigaidi;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa ambayo Wananchi wa Tanzania wanapata kutokana na kujiunga na IMO na ESAAMLG na kutokana na manufaa ambayo watapata kutokana na Itifaki hii, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Itifaki ya Uzuiaji wa Vitendo Haramu dhidi ya Usalama wa Miundombinu ya kudumu iliyojengwa chini ya Bahari katika Mwambao wa Bara Mwaka 1988.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 24 Novemba, 2014.

Dkt. T. D. Kashililah
KATIBU WA BUNGE